**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UZINDUZI WA WIKI YA HUDUMA ZA KIFEDHA KITAIFA

**TAREHE 24 NOVEMBA, 2022**
**MWANZA**

***Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango;***

***Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar;***

***Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo;***

***Mhe. Meja Jenerali Suleiman Mungiya Mzee, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mwanza;***

***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;***

***Ndg. Emmanuel Tutuba, Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango;***

***Dkt Juma Malik Akil, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar;***

***Makatibu wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wote;***

***Prof. Florens Luoga, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania;***

***Dkt. Baghato Saqware, Kamishna wa Mamlaka ya Bima Tanzania;***

***Ndugu Nicodemus D. Mkama Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji Tanzania;***

***Wakuu wa Taasisi za Fedha, Program na Mifuko ya Serikali ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi;***

***Viongozi wa dini;***

***Waandishi wa Habari;***

***Ndugu Washiriki wa Maonesho ya Wiki ya Huduma za Fedha;***

***Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana.***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…**

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia afya njema na ridhaa ya kuhudhuria uzinduzi huu wa **Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha** yanayofanyika hapa Jijini Mwanza. Ninatoa pia shukrani zangu za dhati kwa **Waziri wa Fedha na Mipango** kwa kunialika katika tukio hili muhimu. Vilevile, naipongeza Kamati ya Maandalizi, wadau wote wa Sekta ya Fedha, wakiongozwa na **Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania,** kwa kufanikisha Maadhimisho haya. Nawashukuru Wageni Waalikwa na Wananchi kwa ujumla kwa kujumuika nasi katika tukio hili muhimu.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Kama wote mnavyofahamu, huduma za kifedha zinajumuisha huduma za kibenki za kupokea amana kutoka kwa mwananchi mmoja mmoja, vikundi na makampuni; ukopeshaji wa fedha kwa wateja na ulipaji wa mikopo; kuendesha mfumo wa riba za amana na mikopo; kuwezesha mauzo na

manunuzi; ubadilishaji wa fedha za kigeni; na utumaji na upokeaji wa fedha. Huduma nyingine za kifedha ni pamoja na huduma za bima, uendeshaji na usimamizi wa masoko ya mitaji na dhamana, na huduma za ushauri kuhusu biashara na uwekezaji na uchaguzi wa madirisha ya kuwekeza mitaji (Wealth Management). Huduma hizi pia ni chanzo muhimu cha mapato ya Serikali. Hivyo, huduma za kifedha ni mhimili muhimu sana wa uzalishaji, ufanyaji biashara, uwekezaji na kukuza uchumi na pia kuwezesha uendeshaji wa Serikali. Ni dhahiri pia kuwa huduma za kifedha ni mtambuka na pia ni chachu ya maendeleo ya Taifa na ustawi wa maisha ya wananchi kwa ujumla. Hivyo kama kaulimbiu ya Maadhimisho haya inavyosema "***Elimu ya Fedha kwa Maendeleo ya Watu***", hatuna budi kuhakikisha wananchi wana ufahamu wa kutosha kuhusu fursa na huduma mbalimbali za fedha zilizopo katika soko na namna wanavyoweza kuzifikia ili wazitumie kujiletea maendeleo. Na hili ndiyo lengo la kufanya maadhimisho haya.

***Waheshimiwa Viongozi na Washiriki***

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa pamoja na mambo mengine, umejielekeza katika kuongeza upatikanaji na matumizi ya huduma rasmi za benki na malipo; kulinda maslahi ya watumiaji huduma; na kubuni bidhaa za benki na mifumo ya malipo kulingana na mahitaji ya soko, mabadiliko ya uchumi na teknolojia. Pamoja na Mpango huo wa Maendeleo wa Taifa, Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (2021/22-2029/30); na Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano wa Elimu ya Fedha (2019/20-2025/26) imeweka msukumo wa kipekee katika kuimarisha huduma za fedha na ufahamu wa huduma hizo kwa kila mwananchi.

***Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Naungana na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kuyatambua mafanikio makubwa ya Sekta ya Fedha nchini licha ya misukosuko iliyosababishwa na janga la UVIKO-19. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Fedha, Serikali inatambua uwepo wa changamoto mbalimbali ambazo hatuna budi kuzitafutia ufumbuzi. Kwa mfano, bado baadhi ya Watanzania hususan waishio vijijini hawajafikiwa na huduma za fedha. Kwa mfano ni asilimia 8.6 tu ya wananchi waishio vijijini wanapata huduma za benki kwa sasa. Halikadhalika, masharti na riba za mikopo bado sio rafiki na ni mzigo kwa walio wengi kuweza kunufaika na mikopo wanayopewa. Changamoto nyingine ni kiwango cha upatikanaji na elimu ya Huduma za Bima hususan za kilimo cha mazao na ufugaji bado ni cha chini, hali inayopelekea uwekezaji mdogo katika sekta hiyo muhimu.

Natambua jitihada zinazofanyika za kutatua changamoto hizo. Kwa mfano, mmenieleza hapa kwamba mmepanga kutumia kiasi cha takribani shilingi bilioni 133.3 kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ikiwamo kuwapatia mitaji,

kutoa mafunzo, na kuongeza matumizi ya TEHAMA kwenye sekta ya fedha. Natambua pia, jitihada za Benki Kuu ya Tanzania kusaidia sekta ya kilimo kupitia Mfuko maalum unaokopesha benki za biashara na taasisi nyingine za fedha kwa riba ya asilimia 3 ili kuziwezesha nazo kutoa mikopo nafuu kwa wawekezaji katika sekta ya kilimo. Matokeo ya uwekezaji huo yameanza kuonekana ambapo benki kadhaa zimeweza kukopesha wakulima kwa riba ya asilimia 9.

Natambua vilevile jitihada za kuongeza wigo wa huduma za fedha zinazofanywa na benki/taasisi moja moja. Jitihada hizo ni pamoja na hatifungani inayokidhi matakwa ya maadili ya Kiislam (*Sukuk Bond*); hatifungani ya benki ya NMB (*Jasiri Bond*) kwa ajili ya kuendeleza sekta ya nyumba na makazi; hatifungani ya Kampuni ya *Afrisian Ginning Limited* kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha pamba; na hatifungani ya NBC (*NBC Twiga Bond*) kwa ajili ya kuwakopesha wajasiliamali wadogo na wa kati.

***Ndugu Viongozi na Wadau wa Huduma za Fedha;***

Ni matarajio yangu kuwa, katika wiki hii ya Maadhimisho ya Huduma za Kifedha, mtaongeza ufahamu wa wananchi wetu na kuweka mikakati ya namna ya kutatua changamoto na kuboresha zaidi huduma za fedha ili zisaidie kuongeza kasi ya maendeleo ya Watanzania. Kwa muktadha huo napenda kusisitiza na kuelekeza mambo yafuatayo:

**Jambo la Kwanza**, Kwa muda mrefu sasa mchango wa Sekta ya Fedha katika Pato la Taifa umekuwa chini ya asilimia 4 (yaani asilimia 3.4, 3.5, 3.5 na 3.8 kwa mwaka 2021, 2020, 2019, 2018, mtawalia). Hatuna budi kubadilisha mwelekeo huu, ukizingatia jitihada mbalimbali zilizowekwa hadi sasa. Hivyo, naitaka Wizara ya Fedha na Mipango (Bara na Visiwani) kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, Umoja wa Mabenki Tanzania (Tanzania Banker's Association) na Wadau wote mnaoshiriki Maadhimisho haya, mfanye tafakuri ya kina kuhusu namna ya kuongeza ubunifu ili Sekta hii iweze kuchangia zaidi katika jitihada za kupunguza umasikini na maendeleo ya Watanzania. Napenda nitaje maaneo machache ambayo naamini ni vyema yakazingatiwa:

(i) Riba ya mikopo ya wastani wa asilimia 16 bado ni mzigo kwa Watanzania walio wengi kumudu. Hivyo, pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa kupunguza hatari za kifedha (financial risks) ninasisitiza kila benki kupitia umoja wenu (TBA) mchambue mizizi ya changamoto hii na kupunguza zaidi riba kwa wakopaji. Pigeni darubini gharama zenu za uendeshaji na matumizi mengine kama bonasi n.k. Serikali imekuwa ikitoa rai hii kwa muda mrefu sana lakini mwitikio wa mabenki bado ni mdogo mno kuweza kuwavutia wananchi walio wengi wa kipato cha chini na kati kukopa na kurejesha mikopo;

(ii) Tazameni pia upya masharti ya mikopo, ikiwamo dhamana ya mali zisizohamishika kwa kuwa ni kikwazo kwa wajasiliamali wetu – je hakuna mbadala? Angalieni uwezekano wa kutumia historia nzuri za wakopaji (credit scores) katika Credit Reference Bureaux kama dhamana;

(iii) Vijana ambao ni sehemu kubwa ya nguvukazi ya Taifa letu bado huchukuliwa kuwa ni soko gumu kwa huduma za fedha. Hivyo, ninawataka mje na mbinu mpya na bunifu (creative interventions) za namna ya kulifikia soko hili kubwa; na

(iv) Gharama za kutuma/kupokea pesa kimataifa na za matumizi ya *credit/debit cards* ziko juu. Hali hii imesababisha wageni na Diaspora wetu kutumia njia zisizo rasmi wanapowatumia pesa jamaa zao hapa Tanzania. Kwa upande wa *credit cards*, tozo za benki au mawakala wao ni mzigo, zinakwamisha watalii kununua vitu vyetu kwa wingi na hivyo kuikosesha mapato Serikali na watoa huduma mbalimbali. Hivyo, ni muhimu benki ziongeze ubunifu ili huduma hizo zitolewe kwa gharama nafuu au angalau zilingane na viwango vya kimataifa*.*

**Jambo la Pili**, Taarifa yenu inaonesha ni asilimia 8.6 tu ya wananchi waishio vijijini wanapata huduma za benki kwa sasa. Nautaka Umoja wa Mabenki Tanzania (TBA), msaidie kuhamasisha wanachama wenu kutanua wigo wa huduma zao vijijini. Hamna budi kuongeza mitaji yenu ili mkopeshe zaidi; na kukuza akiba ili kupunguza utamaduni wa watu kutunza pesa kwenye vibubu. Serikali imeboresha miundombinu; Benki Kuu ya Tanzania imelegeza masharti ya usajili wa huduma za Mawakala wa benki; na teknolojia ya kidigitali imekuwa ni nyenzo ya kipekee kuwafikia wananchi wengi zaidi. *Tusibweteke na ukuaji wa amana wa asilimia 13 tulioupata katika kipindi cha mwaka 2020/2021. Bado mikoa kama ile ya Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini ina mchango mdogo katika amana za benki (chini ya asilimia 9 kwa mwaka 2019/20, 2020/21 na 2021/22) licha ya kuwa na shughuli nyingi za kiuchumi.*

**Jambo la Tatu**, Mwezi Septemba 2021 Tanzania iliridhia kujiunga na Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) lenye soko la watu takribani bilioni 1.4. Ushiriki wetu katika soko hili unategemea sana gharama za ubadilishaji wa sarafu zetu (*currency convertibility*). Natambua kuna mwitikio mdogo miongoni mwa wadau wa Huduma za Fedha hususan benki zetu kutumia mifumo ya kikanda iliyowekwa kurahisisha malipo na ubadilishaji wa sarafu. Napenda kuwashawishi mtumie mifumo kama vile *East African Payment System na SADC Integrated Regional Electronic Settlement System* ili kuwapunguzia wafanyabiashara wetu gharama za kubadili sarafu na hivyo kuchochea biashara za kikanda.

**Jambo la Nne**, Kama nchi tumefanya kazi nzuri ambapo matumizi ya huduma jumuishi za fedha kwa njia ya simu za mkononi imeendelea kuongezeka kufikia akaunti milioni 33.1 mwaka 2021 kutoka akaunti milioni 30.3 mwaka 2020. Na katika kipindi kama hicho, miamala ya huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi ilikuwa na thamani ya shilingi trilioni 9.2 mwaka 2021 na shilingi trilioni 11.1 mwaka 2020. Hata hivyo, pamoja na mafanikio haya, napenda niwasisitize Benki Kuu ya Tanzania na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) mhakikishe watoa huduma wanaheshimu Sheria ya Kumlinda Mtumiaji. Sote ni mashahidi kuwa, riba au gharama zinazotozwa na baadhi ya watoa huduma kutokana na mikopo ya muda mfupi (ya fedha au muda wa maongezi) ni kubwa mno - asilimia 30-100. Pia wananchi waelezwe makato yao kabla hawajaamua kuchukua mikopo hiyo.

***Jambo la Tano***, Nawataka wadau wote wa huduma za fedha kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira; na Wizara ya Fedha na Mipango; na Ofisi zetu za Ubalozi, kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuchangamkia fursa na rasilimali za kimataifa katika kulinda mazingira (mfano: *Green Climate Fund*). Naipongeza Benki ya CRDB kwa kujiongeza na kunufaika na fursa hizo. Sote tuige mfano huo ili tuweze kupata fedha za kusaidia jitihada za Serikali katika kuhifadhi mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

***Jambo la Sita***, Napenda niwakumbushe Wakufunzi kuwa katika Maadhimisho haya waelimisheni wananchi kuhusu kuibuka kwa wimbi la fedha za kidigitali (*yaani, Central Bank Digital Currency, cryptocurrencies, au bitcoins n.k.*). Benki Kuu ya Tanzania, saidieni kutoa elimu na mwongozo kuhusu fursa na hatari zinazoambatana na maendeleo hayo ambayo yanaigusa jamii yetu hususan vijana na baadhi ya wastaafu wetu wenye kiu ya kuwekeza huko.

***Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwashukuru Watanzania wote mliojumuika nasi katika uzinduzi wa Maadhimisho haya. Nawasihi mtumie vyema fursa hii kuzielewa vyema huduma mbalimbali za fedha na hatimaye mzitumie. Aidha, naipongeza sana Kamati ya Maandalizi kwa kazi nzuri ya uratibu na maandalizi ya hafla hii ya ufunguzi.

Baada ya kusema haya, **ninayo furaha kubwa kutamka kuwa, Maadhimisho ya Pili ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa kwa mwaka 2022, yamefunguliwa**.

**HUDUMA ZA KIFEDHA OYEE!**

**TANZANIA OYEE!**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**